

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA NANE

07 NOVEMBA, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA NANE – TAREHE 07 NOVEMBA, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

124. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Zahanati katika Kata ya Binza – Maswa.

125. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaboresha Kituo cha Afya Mtina ili kitoe huduma za upasuaji.

126. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (BABATI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi Babati ambayo ni Stendi Kuu ya Mkoa wa Manyara.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

127. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, nini husababisha kuchelewa kubadilishiwa Muundo wa Utumishi kwa Walimu mara baada ya kujiendeleza Kitaaluma.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

128. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, utekelezaji wa Mradi wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kupitia mifumo Ikolojia Wilaya ya Kaskazini "A" Zanzibar umefikia wapi.

WIZARA YA UJENZI:

**129. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL
MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini mchakato wa kumpata Mkandarasi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba utaanza ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

**130. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY
(MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti ukuaji wa makazi katika maeneo ambayo hayajapimwa na kupangwa kuwa Makazi ya Wananchi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

131. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Raia wa Kigeni hawashiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

132. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia ya Tshs. 236,000,000 kwa Wananchi wanaopisha ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Nyang'hwale.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

133. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itafungua na kuanza kutumia lango la Kaskazini la Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi lililojengwa Ndea - Mwanga.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
07 NOVEMBA, 2024**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**